

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA NNE

08 APRILI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA NNE – TAREHE 08 APRILI, 2026

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

21. MHESHIMIWA AISHA MSANTU MDUYAH (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Serikali itaridhia na kuanza utekelezaji wa Itifaki ya Afrika kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu (*African Disability Protocol*).

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

22. MHESHIMIWA ENG. FADHILI SANDALI CHILOMBE (TUNDURU KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara za kuunganisha Vijiji vilivyoanzishwa toka Mwaka 1974 katika Jimbo la Tunduru Kusini.

23. MHESHIMIWA DEVOTHA DANIEL MBURARUGABA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, hatua gani inachukuliwa kuhakikisha usimamizi, utoaji, urejeshaji wa Mikopo 10% ya Halmashauri unakuwa wazi na unawafikia walengwa.

24. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Mnadani.

OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

25. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIM HALAMGA (HANANG’):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, kwa nini Serikali isipitie upya Mkataba wa Shamba la Basout la Ngano *Limited* lenye Ukubwa wa Ekari 43,000 ambalo limekuwa pori.

WIZARA YA UJENZI:

26. MHESHIMIWA ALAN THOMAS MVANO (KAKONKO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya Kakonko kwenda Mpaka wa Muhange kupitia Gwarama km 41.43 itajengwa kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

27. MHESHIMIWA EDIBILY KAZALA KINYOMA (KASULU VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni kwa kiasi gani Wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini wananufaika na uwepo wa Mwekezaji wa Kitalu cha Makere *Forest Reserve*.

WIZARA YA MAJI:

28. MHESHIMIWA TWAHA SAID MWAKIOJA (MKINGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itawapatia maji safi na salama Wananchi wa Wilaya ya Mkinga kupitia Mradi wa Tanga - Horohoro.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

29. MHESHIMIWA SULEIMAN MOHAMED RASHID (MWERA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi Na Teknolojia:-

Je, Serikali imejipangaje katika utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 Toleo la 2023.

WIZARA YA UCHUKUZI:

30. MHESHIMIWA KIZA HUSSEIN MAYEYE (KIGOMA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa Bandari ndogo ya Kagunga na Soko la Kagunga utakamilika ili kuimarisha biashara kati ya Tanzania na Burundi.

31. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Hoteli katika Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

32. MHESHIMIWA ZUBERI YAHYA MFAUME (MOROGORO KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itaingilia kati na kudhibiti migogoro ya ardhi kati ya Wakulima na Wawekezaji wa Morogoro Sugar.

WIZARA YA FEDHA:

**33. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL
SICHALWE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Kituo cha Forodha katika Jimbo la Momba kitaanza kujengwa.

WIZARA YA AFYA:

**34. MHESHIMIWA DKT. CATHERINE CANUTE
JOACHIM (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mpango gani wa kuendeleza Utalii wa Tiba nchini ili kuboresha huduma za Afya na kuongeza mchango wa Sekta ya Afya katika pato la Taifa.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**35. MHESHIMIWA DICKSON NATHAN LUTEVELE
(MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini malipo ya waliokuwa Wafanyakazi wa Kiwanda cha Karatasi (SPM Mgololo) yatafanyika ukizingatia kuwa ni ya muda mrefu sana.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

(Majadiliano yanaendelea)

DODOMA
08 APRILI, 2026

BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE